



**The International Small Group and
Tree Planting Program**

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd.

**New Group Information Packet
In Swahili**

Revised: February 16, 2004

Karibu Katika Mradi Wa TIST	2
Historia Ya TIST	3
Makubaliano Ya Kunufaisha Vikundi Vidogo Vidogo	5
Fomu Ya Kujiandikisha	6
Utaratibu wa vikundi vilivyosajiliwa.....	7
Karatasi Zenye Kuelezea Ukweli Halisi Juu Vikundi Vya TIST	13
Small Group Account Statement and Payment Voucher	22
Greenhouse Gas Sale Agreement.....	23
Emission Reduction Credit Notice.....	25

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd The International Small Group and Tree Planting Program Karibu Katika Mradi Wa Tist

Karibu katika mradi wa TIST! Tunawaletea salamu wanachama wote wa kikundi kutoka kwa wote wanaosaidia mradi huu wa TIST.

Tunayofuraha kwa kikundi chenu kuamua kujiunga na vikundi vingine vingi katika mradi huu wa TIST. TIST ni mradi unaokuwa haraka na unaofanya kazi Ulimwengu mzima.

Vikundi vinavyofanya kazi katika mradi huu wa TIST vinafanya mabadiliko katika Mazingira. Vikundi vidogo vya mradi huu vimesha panda miti zaidi ya milioni 2.4 katika nchi za Tanzania na India!

Kila wiki vikundi vipya kama cha kwenu hukusanyika katika nchi mbalimbali. Wanachama wake Wanasaidiana wao kwa wao. Wanapanga jinsi ya kuanzisha vitalu, kupanda miche, na kuandaa sehemu za kupanda miti, na kuboresha bora katika mambo ya kilimo. Wanaziendeleza na kushirikishana njia mbalimbali wanazozigundua kutoka katika vikundi vingine.

Tunamatumaini kuwa kikundi chenu kitaleta mafanikio na kuboreka na faida zilizoko kwenye mradi wa TIST. Tunashauku ya kusaidia kikundi chenu. Tuelezeni ni mambo gani mngeyahitaji na ni mafunzo gani yatasaidia kikundi chenu. Muwe huru kueleza ni mambo gani yanaweza kuboresha mradi. Kupitia njia hii ya kushirikishana wanachama wote wa mradi hii Ulimwenguni kote watanufaika na faida mtakazojifunza.

Kitu cha kwanza kufanya ni wanachama wa kikundi kukutana kila wiki. Katika kikundi chenu mnapaswa kusoma utaratibu wa Mradi ambao mtapewa na Mratibu wa Mradi na kuulewa.

Tafadhali Muoneni Mratibu wa mradi wa TIST endapo utakuwa na swali lolote au tatizo. Pia unaweza kuandika kwetu: Kupitia Mtandao kwa kutumia Internet café au mtu yeyote anayetumia E-mail tumia anuani ifuatayo info@tist.org tutafurahi sana kupata maoni au lolote kutoka kwenu!

Tunawashukuru na Kuwajali,

The International Small Group and Tree Planting Program HISTORIA YA TIST

TIST ni Mradi wa maendeleo ya upandaji miti na kuinua uchumi. TIST inafanya kazi na vikundi vinavyotaka kupanda miti mingi ili kuboresha mazingira na kusaidia kuinua kipato cha kifedha. TIST hivi sasa inafanya kazi Katika nchi mbalimbali. Kupitia vikundi vingi katika maeneo mengi, historia hii- na Miti ya TIST.. itaendelea kukua!

July-August 1998 na 1999

- Mission Teams Kutoka Marekani wakialikwa na Kanisa Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa Tanzania. Walitoa semina ya mafunzo ya Uongozi wa vikundi vidogo vidogo kupitia masomo ya Biblia, katika kusaidiana na Uanzishaji wa vikundi
- “Njia Bora” Kuna njia Zilizogunduliwa kwenye semina hiyo na washiriki wa semina pamoja na mission team
- Masomo ya Biblia, Kusaidiana, na Uanzishaji wa vikundi vilivyopangiliwa

August 1999

- Upanuzi wa mafunzo ya Uongozi wa Vikundi vidogo vidogo na Utoaji wa semina za Ufundishaji wa walimu wa vikundi vidogo vidogo
- Semina ambayo washiriki waligundua mahitaji maarumu na malengo kwa Dayosisi na nchi yao:
 - Kuboresha mazingira yetu kwa kutumia kilimo cha mzunguko na Upandaji miti itakayosaidia kwa matumizi ya kuni na Mkaa.
 - Kupunguza au kuondoa tatizo la Njaa
 - Wawezeshaji au walimu waliofundishwa kutoa mafunzo kwenye vikundi juu ya “Njia Bora” za uendeshaji wa Vikundi

December 1999

- Kulianzishwa vikundi 40 katika Dayosisi ya Mpwapwa na Kampuni ya Clean Air Action Corporation ilianzisha Mradi wa TIST
- “Phase I” Ilianza...

January – March 2000

- Vikundi 40 vilijiunga na kuendeleza Mradi wa TIST

May 2000

- Wawakilishi walichaguliwa kutoka katika maeneo tofauti tofauti kuunda Bodi ya Wadhamini

June- September 2000

- Maendeleo ya semina ya mafunzo ya Viongozi wa vikundi na Mafunzo ya Wawezeshaji wa vikundi
- Mafunzo ya Njia Bora katika Kilimo Hai yalianza kwa vikundi vidogo vidogo
- Jarida la kwanza la *Habari Moto Moto* linalotoka kila Mwezi lilitawanywa kwenye vikundi
- Phase I Ilikwisha, Phase II Ilianza...

January – October 2001

- Kuliongezeka idadi ya vikundi 472 ambavyo vilijiunga na Mradi wa TIST
- Kulitolewa nyongeza ya Mafunzo katika: Upandaji wa miti, Uanzishaji wa vitalu, Utunzaji wa miche kwenye vitalu, Mafunzo ya kilimo Hai

January – Septemba 2002

- Ongezeko la vikundi 140 katika Mradi wa TIST
- Zaidi ya miti 900,000 iliyokuwa hai Ilihesabiwa katika Wilaya za Mpwapwa na Kongwa, Tanzania
- Mradi wa TIST Ulianza Morogoro, Tanzania
- Mradi wa TIST Ulianza vijiji vilivyoko karibu na Chennai, India
- Vikundi 51 vilianzisha vitalu
- Phase II Ilikwisha! Na Phase III Ilianza...

January – June 2003

- Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania Ltd. (UMET) iliandikishwa ilikuendesha mradi wa TIST Tanzania
- TIST ilianza Kibondo, Tanzania

TIST Welcome Packet/Swahili

- Utaratibu mpya wa kutumia Hundi (Vocha) maarum ilianza kufanya kazi kwa vikundi vya awali vya TIST

July – Octoba 2003

- Tukio la mafunzo ya kimataifa yalifanyika ukihudhuriwa na wawakilishi wa nchi 7
- Shughuli za maandalizi ya shughuli za mradi nchini Uganda, Africa Kusini na Kenya yalifanyika

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd (UMET) The International Small Group and Tree Planting Project (TIST) Makubaliano Ya Kunufaisha Vikundi Vidogo Vidogo

Maalezo mafupi.

UMET ina shirikiana na kufanya kazi na vikundi vidogo vidogo vyenye watu kati ya 6 mpaka 12, wenye nia ya kuboresha mazingira yao na kuongeza kipato kwa kupanda miti. Hivi vikundi vinatayarisha miche ya miti na kupanda katika maeno yao. UMET itafanya malipo ya Shs 4/= kila baada ya miezi mitatu kwa muda unaoweza kufikia miaka 50 kwa kila mche au mti ulio hai. Miti hii ni mali ya vikundi vinaweza kupata matunda, vinaweza kutumia baadhi ya miti kwa kuni au kupasua mbao. Pia vikundi vinaweza kufanya biashara mpya ya kuuza bidhaa inayoitwa "Carbon credit" inayohusika usafishaji wa hewa kutokana na miti. Yafuatayo ni mambo ambayo kikundi kinapaswa kufanya ili kujiunga na mradi. Na faida watakazoweza kupata.

Kikundi kifanye shughuli zifuatazo.

- Kukubali kwa maandishi makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja kwa muda usiopungua miaka mitano.
- Kikundi kikutane mara moja au zaidi kila wiki.
- Kikundi kikutane na vikundi vingine katika kijiji chao mara moja kwa mwezi.
- Kiotesho miche 1000 au zaidi kabla ya mwezi Agosti kila mwaka.
- Kitafute maeneo kwenye mashamba, karibu na nyumba, kando kando ya njia, kanisani kwa ajili ya kupanda miti.
- Kuandaa mahali pa kupanda miti pamoja na kuchimba mashimo.
- Kupandikiza miche kwenye mashimo mwanzoni mwa msimu wa mvua.
- Kupalilia miti (na kuimwagilia kama inahitajika) mpaka miti itakapofikia angalau muda usiopungua mwaka mmoja.
- Kusaidia kuhesabu miti.
- Kurudisha fomu za taarifa za kila mwezi.
- Kufungua akaunti ya kikundi kwenye benki iliyo karibu.
- Kuhamishia usafishaji wa hewa taka (Greenhouse gas credit) kutoka kwenye miti na kuweka kwenye UMET.
- Kutayarisha miche zaidi na kupanda miti mingi zaidi kila mwaka.

Vikundi vitapata faida nyingi.

- Kikundi kitamiliki miti hiyo.
- Miti itawapatia wanavikundi, vivuli, kuni, mbao, kurutubisha udongo, matunda, mbegu za mafuta –mfano korosho, dawa, malighafi za kutengenezea vinyago, vinu n.k.
- UMET itaweka Tsh 4/= kwa kila mche au mti ulio hai, kila baada ya miezi mitatu katika akaunti ya kikundi. Kadiri kikundi kitakavyokuwa na ongezeko la miti ndivyo kipato chao kitaongezeka
- UMET itasaidia kutoa mafunzo ya kibiashara, utunzaji wa fedha, kilimo hai na mambo mengine yanayoweza kuwasaidia wanavikundi katika vijiji vyao.
- UMET itavisaidia vikundi kuuza "Greenhouse gas credit".

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd
The International Small Group Tree Planting Program (TIST)
Fomu Ya Kujiandikisha

TIST ni Mradi wa maendeleo ya upandaji miti na Uchumi
TIST Inafanya kazi katika _____ Na _____.

Kikundi kidogo kinaweza kuwa na wanachama 6-12. Kikundi kidogo kinaweza kuandikishwa kuwa katika Mradi wa TIST endepo kitasoma na kuelewa Karatasi za makubaliano ya Vikundi vidogo vidogo na kukubaliana na yale yanayohitajika

Jina la kikundi _____

Kijiji _____

Tarehe ya Leo _____

Jina :	Sahihi:	Male/Female	Age
1. _____	_____		
2. _____	_____		
3. _____	_____		
4. _____	_____		
5. _____	_____		
6. _____	_____		
7. _____	_____		
8. _____	_____		
9. _____	_____		
10. _____	_____		
11. _____	_____		
12. _____	_____		

Kama kikundi tayari kina namba ya Akaunti ya Banki:

Namba ya Akaunti ya Banki: _____

Jina la Tawi na Bank _____

Sehemu hii iliyobaki itajazwa na Mratibu

Eneo la (Center Code) ya Kikundi _____

Namba ya TIST _____

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania The International Small Group and Tree Planting Program Utaratibu wa vikundi vilivyosajiliwa

Utangulizi

Hongera kwa kusajiliwa kama kikundi katika mradi wa TIST. Maelezo haya yanafafanua hatua ambazo vikundi vinapaswa kufuata ili kunufaika na mradi huu wa TIST. Kila mwanakikundi anapaswa kusoma na kuelewa maelezo haya. Tafadhali muulize mratibu wa mradi wa TIST katika eneo lako swali lolote linalohusu maelezo haya

Kusoma Na Kuelewa Maelezo Ya Ukaribisho

Sasa kikundi kimesajiliwa na TIST nadhani unahamu kujua nini kitafuata katika maelezo ya ukaribisho kwa TIST, utapata ufafanuzi wa kutosha. Maelezo haya yanafafanua hatua muhimu za mradi wa TIST. Kwa mfano

- Namna ya kuchagua na kutafuta mbegu na miche ya miti
- Namna ya kutunza vitalu vya miche
- Namna ya kuandaa shamba na kupandikiza miche ya miti
- Jinsi ya kufanya kazi katika vikundi kwa ufanisi
- Namna ya kusimamia mapato yatokanayo na TIST na namna ya kuanza kilimo Hai cha utunzaji wa mazingira

Mratibu wa TIST katika eneo lako atatoa ufafanuzi wa maelezo haya. Baada ya haya ufanisi wa kikundi wote ni muhimu wasome kwa uangalifu maelezo yote na kuyaelewa kwa kina.

Ni muhimu kumuuliza mratibu wa tist katika eneo lolote unaloweza kuwanalo juu ya maelezo hayo.

Picha Ya Kikundi

Baada ya kikundi chako kusajiliwa mratibu wa TIST katika eneo lako atapiga picha ya kikundi chako ikiwa na wanakikundi wote. Panga muda na mratibu wa TIST katika eneo lako na hakikisha wanakikundi wote wamehakikisha wakati wa kupiga picha hiyo.

Kuanzisha Shughuli Za Vikundi

Wanavikundi hufanya kazi za TIST kwa pamoja, wanavikundi wanahamasishana. Wanakikundi wanahakikisha kila mmoja anafanya shughuli ile waliokubaliana. Kila mwanakikundi anamawazo mazuri ya kuchangia kwa wenzake. Vikundi vyote vya TIST vitafanya kazi kwa ufanisi miongoni mwa wanakikundi wake kwa kufuata misingi ya maelekezo kama ilivyotolewa katika maelekezo ya utendaji kazi. Hii itahusisha kukutana maramara na kutunza kumbukumbu za mikutano na shughuli zingine za kikundi.

Kikundi kinaweza kubadilishana mawazo na kikundi kingine juu ya yale waliojifunza. Hii ni sababu mojawapo ya TIST kufanya vizuri. Waratibu wa mradi haatakuieleza kila kitu cha kufanya, TIST itawezesha upatikanaji wa habari na vikundi vingine duniani.

Utunzaji Wa Vitalu

Sasa ukotayali kuanza kazi kama kikundi cha TIST.

Ni muhimu kuanza kwa kuchagua aina ya miti ambayo ungependa kupanda na kutafuta mbegu zake. Tafadhali rejea kitini cha mbegu na miche ya miti kwa ajili ya misingi ya kuchagua na kutafuta mbegu. Mara upatapo mbegu anza kutengeneza kitalu. Utakapo siha mbegu katika viriba tafadhali rejea kitini cha ukuzaji na utunzaji wa kitalu kwa ajili ya mbinu bora za utunzaji wa kitalu.

Fomu Za Taarifa Za Kila Mwezi

Moja ya wajibu wa kikundi chenu ni kuipatia TIST taarifa ya kila Mwezi.

Katika kitini cha ukaribisho kuna nakara sita za fomu za kutoa taarifa za kikundi kila mwezi. Fomu hii itakuwa ya muhimu kwa kufikisha taarifa za kikundi Ofisi ya TIST. Kila mwisho wa mwezi mtajaza taarifa za mwezi kuelezea taarifa za kikundi chenu katika kipindi cha mwezi mzima kilichopita.

Ilikujaza fomu hii :

- 1 Weka kumbukumbu ya vikao vya kikundi chenu kila mwezi
- 2 Hesabuni miche na miti iliyopandwa ya kikundi chenu kila Mwezi
- 3 Jazeni taarifa hiyo ya mwezi ya kikundi siku ya mwisho ya kila mwezi.
- 4 kuwe na wanakikundi wanne wa kusaini kila fomu ya taarifa ya mwezi.

Jaza fomu moja kila mwisho wa Mwezi;

Muwe makini wakati kuhesabu miti na miche. TIST itafanya malipo kulingana na idadi ya miti na miche iliyopo kwenye fomu ya taarifa ya kila mwezi. TIST itafanya ukaguzi wa miti na miche iliyopandwa ilikuhakikisha kuwa idadi iliyotolewa taarifa iko sahihi. Taarifa yoyote ambayo haiko sahihi au ya uongo itapelekea kuwepo na faini katika malipo ya miti au kikundi kufutwa kutoka kwenye mpango wa TIST. Mratibu wa TIST atakusanya taarifa ya kila mwezi. Mfano taarifa ya mwezi wa Kumi imfikie Mratibu kabla ya tarehe 7 November au Wakati mratibu anapokuja kwenye Vituo maarum (Node meeting) kulingana na ratiba, vikundi viwakilishe fomu zao. Muulize mratibu wa TIST ni ratiba ipi itatumika ilikuvifikia vikundi na kuchukua fomu za taarifa ya kila mwezi. Pia ratiba hiyo inawezakutolewa kwenye HMM. Mratibu atachukua fomu hizo na kuingiza kwenye komputer na kuingiza kwenye mtandao na kutuma taarifa.

Mnatakiwa kumpatia mratibu wa TIST fomu moja ya taarifa ya kila mwezi kwa miezi 3 mfululizo ilikupata malipo yenu kwa wakati muafaka. Kama mtachelewesha bado mtaweza kupata malipo lakini yatakuwa yamechelewa. Hakikisheni kuwa mratibu anawapatia fomu za taarifa za mwezi zisizojazwa za kutosha.

Malipo Kutokana Na Miche Na Miti.

TIST itafanya malipo kwa miche na miti iliyohai mliyonayo, kama ilivyofafanuliwa katika kitini. Malipo yatafanyika mara moja kila baada ya robo mwaka (miezi 3) na yatazingatia takwimu za miche na miti itakayotolewa kwenye taarifa ya kikundi ya kila mwezi. Ili TIST ifanye malipo ya kila robo mwaka ni muhimu mfungue akaunti katika bank iliyokaribu. Malipo kutoka TIST yatafanyika baada ya vikundi kufungua akaunti.

TIST itawapatia Vocha au Hundi ambayo mtaipeleka Bank na kuwekewa fedha kwenye akaunti yenu.

Kikundi chenu ni lazima kiwe na akaunti Bank ilikutumia Vocha au Hundi hiyo. Hizi hapa ni hatua za kufuata

- 1 Muulize mratibu kuwa ni Benk ipi ya kutumia
- 2 Tembeleeni Benk na muwaulize maafisa wa Benk jinsi ya kufungua akaunti ya kikundi.
- 3 Fungueni akaunti ya kikundi ambayo itaendeshwa kwa umoja na wanavikundi wote
- 4 Muwaulize watumishi wa Benk jinsi ya kuchukua fedha/kuweka n.k

Hakikisha kuwa wanavikundi wote wanaelewa jinsi ya kuishughulikia akaunti ya kikundi.

Kila baada ya miezi mitatu utapata hati ya maelezo kutoka TIST. Kama umekwisha rudisha fomu tatu za taarifa ya mwezi kwa kipindi cha miezi 3 mfululizo, Hati hiyo pia itakuwa imeambatanishwa na Vocha.

Kama hukurudisha fomu tatu za taarifa ya mwezi kwa wakati muafaka, basi TIST haitakuletea Vocha au Hundi mpaka hapo utakaporudisha fomu za miezi hiyo iliyokosekana. Vocha mpya ya kipindi kinachofuata itajumlisha malipo yote ya awamu mbili, mapya na yale ya mwanzo.

Kikundi chenu kiamue kuiweka Vocha au kuipeleka Benk mara tu mtakapoipata ilimuingize fedha kwenye Akaunti ya kikundi. Pindi mtakapowapatia Benk, wao wataitumia Vocha kuhamishia fedha kutoka akaunti ya TIST kwenda akaunti yenu. Fuateni maelezo yafuatayo kabla ya kupeleka Vocha Benk.

- 1 Ipitieni Vocha wanavikundi wote na kuhakikisha kuwa ipo sahihi.
- 2 Ulizeni swali lolote kwa mratibu wa TIST wa eneo lenu kama kuna mahali hamjalelewa.
- 3 Tunzeni Vocha mahali pa usalama mpaka mtakapokwenda Benk
- 4 Pelekeni Vocha zote mnazotaka kuzitumia Benk
- 5 Watu wa Benk wao wataziangalia Vocha zote na kuona kama ziko sahihi na wanaweza kuweka fedha kwenye akaunti yenu.
- 6 Benk watachukua fedha kutoka Akaunti ya mradi wa TIST na kuweka katika Akaunti yenu.
- 7 Fedha sasa itakuwa kwenye akaunti ya kikundi chenu, ninyi mtaamua ni lini mtazichukua na kuzitumia kulingana na maamuzi ya wanakikundi wote.

Vocha ni karatasi iliyomuhimu sana. Yenye thamani ya fedha. Kama ukipoteza au kuiharibu, itakuchukua muda mrefu kuwapatia vocha mpya.

Ukaguzi Siyopangiliwa Na Ule Wa Mwaka

Tist itafanya ukaguzi wa miti uliokwenye utaratibu wa mwaka na ule wa kushitukiza katika vitalu na mashamba ya miti. Ukaguzi huu wa miti wa mara kwa mara wa kushitukiza utafanyika na wawakilishi wa TIST katika maeneo au hata watendaji wa Mradi. Ukaguzi unaweza kufanyika na watumishi walioajiliwa na TIST au na watu wa nje ya eneo lenu. Wakaguzi wanaweza kutumia kompyuta za mkononi pamoja na vyombo vingine vya kisasa kukagua miti au miche yenu mtakayokuwa nayo. Ukaguzi unafanyika ili kuhakikisha ukuaji na maendeleo ya miche na miti yako ili kwamba uhamishaji wa hewa taka yaani Greenhouse Gas pollution reduction uweze kuhakikishwa. Ukaguzi pia unahakikisha kuwa hesabu mnyoitoa kwenye taarifa yenu ya kila mwezi ni sahihi.

Ni vizuri kushirikiana na wakaguzi na kuwasaidia kufanya ukaguzi wao inavyotakiwa kikamilifu. Wanakikundi watawaonyesha wakaguzi maeneo yote ambayo wanakikundi wamepanda miti yote na kuonyesha miche yote ya kikundi. Kama wanakikundi hawatawaonyesha wanakikundi maeneo yote ya miti na miche na kuwafanya wakaguzi wakashindwa kuhesabu miti na miche yote basi inaweza kuathili malipo ya kikundi.

Angalau mwanachama mmoja awatembeze wakaguzi hawa wakati wa kutembelea maeneo ya kikundi ili waweze kuwaonyesha maeneo yote ya kikundi.

Muombe mkaguzi kitambulisho chake ili kujua kuwa hao wameruhusiwa na TIST kukagua miti na miche yako.

Msaidie mkaguzi taarifa muhimu kama jina la kikundi, namba ya kikundi, aina ya miti na miti hiyo ilipandwa lini n.k

Muonyesheni mkaguzi daftari mnaloweka kumbukumbu za kazi za kikundi Wachukueni wakaguzi maeneo yote ya vitalu na mashamba ya miti na maeneo mtakayopanda miti yenu Kagua idadi ya miche au miti iliyokaguliwa. Kama ukiona idadi aliyenayo siyo hiyo kulingana na idadi mliyonayo basi mnaweza kujadiliana ilimpate ukweli.

Weka saini yako kama utakubaliana na ukaguzi wa miche na miti uliyofanyika na Mkaguzi

Wakaguzi wako wapo kwa ajili ya kukusaidia wewe kupata manufaa ya mradi wa TIST na hivyo mnapaswa kuwa na uhusiano mzuri, mshikamano na msaada katika kazi yao. Uwehuru kuuliza swali lolote utakalokuwa nalobila kuwaingilia na katika kazi yao. Kama unawasiwasi na ukaguzi wowote

uliofanyika na Mkaguzi fulani, tafadhali uwehuru kuwasiliana na Mratibu wa TIST na kumuelezea juu ya mambo uliyonayo.

Upandaji Wa Miti

Kadiri miche yako itakavyokuwa mikubwa na kadiri msimu wa mvua utakavyokaribia, ni lazima upange na kuanza shughuli za kupandikiza miche yako kwenye mashimo shambani. Tafadhali rejea kwenye kitini cha uandaaji wa eneo la kupanda miti na kitini cha upandikizaji wa miche ili upate njia sahihi na taratibu za kupanda miti

Upigaji Wa Picha Maeneo Maarumu Ya Kupanda Miti

Eneo lako unalotaka kupanda miti lipigwae picha katika kipindi cha miezi sita baada ya kupanda miti. Picha hizi zinahitajika kuonyesha mchango wa mradi wa TIST katika kuboresha mazingira kwa upandaji wa miti katika maeneo yenu. Hakikisha mratibu wa TIST katika eneo lako anapiga picha za awali katika maeneo yako unayotegemea kupandikiza miche yako. Tafadhali onana na mratibu wako kabla ya kuanza kupandikiza miche yako na kumuomba aje apige picha katika eneo lako. Andika maelezo yote ya shughuli za kikundi chako kwenye daftari na pia eleza kwa kina kwenye taarifa ya kikundi ya kila mwezi.

Kugundua Na Kushirikiana Njia Bora

Moja ya kanuni za mradi wa TIST ni kuviwezesha vikundi kugundua, kupitia uzoefu walionao katika mambo mbalimbali ya mradi, njia bora za asili zinazoweza kusaidia na kutumiwa na washiriki wengine wa mradi. Ugunduaji na ushirikishanaji wa Njia Bora ni dhana yenye nguvu sana na inawawezesha vikundi wanakikundi kugundua kutoka kwenye mikono ya uzoefu na kusambaa kwa haraka sana kwa upana kwa wanavikundi wengine mbali na kutumika kwa wanavikundi wa kikundi fulani tu. Rejea kwenye kitini cha ugunduzi na ushirikishanaji katika kipengele cha ukaribisho na maelezo ya jinsi unavyoweza kugundua na kushirikishana NJIA BORA.

Hatua ya kwanza katika kushirikishana njia bora ni kushirikishana katika kikundi kwa wanachama wenyewe. Ni vizuri mjadili katika vikao vya kila wiki juu ya njia bora zilizogunduliwa na wanakikundi katika kikundi maarumu. Kama mwanakikundi yeyote amegundua njia fulani bora ni vizuri awashirikishe wanavikundi na vikundi vingine pia. Pia utakutana na wanachama wa vikundi vingine na kuwaeleza juu ya njia bora uliyoigundua katika kikundi chenu na pia wanakikundi wa vikundi vingine watawaeleza juu ya njia bora walizozipata katika vikundi vyao. Mratibu wa TIST aliyopo karibu atawapangia mikutano na semina ambazo zitawashirikisha wanavikundi katika eneo lenu. Ni vizuri muongelea na kuziorodhesha njia bora zilizogunduliwa katika semina hizo. Pia ni vizuri kuandika kwa uangalifu njia zote zilizogunduliwa na vikundi mbalimbali mbalimbali na kuzifanyia kazi katika shughuli zenu za vikundi. Pia ni vizuri kurejea kitini chenye njia bora zilizogunduliwa ambacho kimeambatanishwa na karatasi mbalimbali mlizopewa zenye maelekezo ya msingi ambayo ni muhimu sana katika mradi wa TIST.

Jarida

TIST inatoa jarida la kila mwezi linaloandika shughuli zinazofanyika katika maeneo yenu. Habali za jarida hilo zitahusisha habari muhimu kutoka maeneo mengi ya ndani na nje ya nchi, Matangozo ya mambo mbalimbali yajayo, taarifa ya matukio yaliyokwisha kufanyika, Habari mpya na mabadiliko yeyote yatakayojitokeza, Njia bora zilizogunduliwa na vikundi mbalimbali hapa na sehemu zingine, taarifa za vikundi mbalimbali vilivyofanya vizuri, Mfululizo wa mambo yanayofanyika na vikundi kutoka kwenye taarifa za kila mwezi n.k. Hivyo jarida litakuwa ni chombo muhimu cha kupeleka taarifa kutoka kwenye mradi TIST kwenda kwenye vikundi na kutoka kwenye vikundi kwenda kwenye vikundi vingine ndani na nje ya nchi ulimwengu mzima.

Wakati mwingine unaweza kuwasiliana na wafanyakazi wa TIST au wakusanya habari wanaofanya kazi za kuandika taarifa kwa ajili ya jarida ambao wanaweza kuwahoji na kuwapiga picha katika maeneo yenu ya kazi. Tafadhali shiriki kikamilifu na jitihada yeyote na kumbuka kuuliza kitambulisho kwa mtu yeyote atakayesema amehuswa na TIST. Pia kama kikundi chako kina wazo lolote linaloweza kuingia kwenye jarida, usisite kutoa ushauri wa mawazo hayo kwa mratibu wa TIST aliyekaribu nawe, au unaweza kuandika wazo lako hilo kwenye taarifa yenu ya kila mwezi.

Jarida litakuwa tayali kuanzia tarehe 5 ya kila mwezi na unatakiwa kuchukua kwa mratibu aliye karibu na wewe wakati mtakapokuwa mnapeleka taarifa zenu za kila mwezi. Angalau wanakikundi wawili wanatakiwa kuwepo wakati wa kuchukua jarida la kikundi wakiwakilisha wanachama wote wa kikundi. Taarifa za jarida hutolewa katika lugha ya taifa na ile ya kiingereza katika nakala zote.

Msaada Kwa Jamii

TIST itaendelea kufundisha vikundi katika eneo lako. Kuvitumikia vikundi, TIST itatuma wafanyakazi katika mpangilio maarum kwenye maeneo yenu kwa siku chache. Hii tunaita msaada kwa kikundi (community nodes) Node itakuwa ikitembelea na kufanya mzunguko kwenye kikundi chako.

Wafanyakazi wa TIST watakuwa tayari kukusanya na kutoa taarifa katika jamii husika. Vikundi vitatoa taarifa zao za kila mwezi kila mwezi na kukusanya majarida na kupokea taarifa ya idadi ya miti yao na taarifa za akaunti. Vikundi vidogo vitakuwa na nafasi ya kushirikishana Njia Bora na vikundi vingine pamoja na watumishi wa TIST.

TIST itakupatia maelezo zaidi juu ya utendaji wa jamii husika (community nodes) kadiri tutakavyokuwa tunafanya kazi kwa karibu zaidi na mazingira ya mradi.

Kilimohai

Mbali na kuboresha mazingira kwa kupanda miti TIST inawashauri wanavikundi kutumia mbinu za Njia Bora. Kilimo hai huongeza kiwango cha uvunaji wa mazao katika sehemu maarumu ya ekari za shamba. Inasaidia watu kutumia eneo moja kwa kilimo kwa muda mrefu. Rejea kwenye kitini cha kilimo Hai kilichoambatanishwa kwenye karatasi zako kwa maelezo zaidi ya njia na mbinu mpya zilizogunduliwa juu ya haya. TIST inawatia moyo wanavikundi kuchagua angalau eka moja 1) katika ardhi yako iliwe unafanya majaribio ya njia Bora mpya za kilimo zilizogunduliwa. Kikundi kitatakiwa kutoa taarifa ya mbinu za kilimo zinazopatikana na ambazo zanzajaribu na kuona matokeo yanayotokana na shughuli za taarifa za kila mwezi

Vikundi Mama

Tist itachagua vikundi vitakavyokuwa vimewajibika ipasavyo katika shughuli zake kuwa vikundi mama. Vikundi mama vitakuwa na uwezo wa kuanzisha vikundi vipya na kuvifundisha na kuvileya. Vitakuwa na wajibu mkubwa juu ya shughuli ya vikundi hivyo vitakavyokuwa vimeanzishwa. Vikundi mama vitanufaika kwa kupata fedha za bakishishi pamoja na malipo yake ya kawaida kutokana na miti yake. Vikundi mama vitapata asilimia kumi ya thamani ya malipo ya mit na miche yatakayofanya na vikundi vipya vitakavyoanzisha. Vikundi vipya vipata malipo kamili na vikundi mama vitapata ongezeko la asilimia kumi la kiasi kitakachopatikana.

Vikundi fulani vichache vitakavyokuwa vimefanya kazi vizuri ndivyo vitakavyokuwa vikundi mama. Vikundi lazima vifanye vizuri sana upandaji na utunzaji wa miche na miti, kuwasilisha taarifa, kushirikishana vizuri sana kwa vitendo na kufanya kazi ipasavyo katika vikundi.

Kuwa kikundi mama ni kuwa na fedha nyingi zaidi lakini ni kuwa na wajibu mkubwa zaidi. Vikundi mama vitahakikisha usahihi wa takwimu zitakazotolewa taarifa ya vikundi vipya vinavyovilela. Vikundi mama

vitawajibika pia kuhakikisha kuwa vikundi vinavyolelewa vinatunza idadi fulani ya chini ya miche ya miti na miche hai.

TIST itatoa kiundani kuhusu uwajibikaji na motisha kwa vikundi mama ambavyo vitakuwa vimechaguliwa kuwa vikundi mama mwishoni mwa mwaka wa kwanza. Ikiwa mnayomatumaini ya kuwa kikundi mama wanakikundi wa kikundi chenu hakikisheni kuwa kikundi chenu kinafanya vizuri sana katika mwaka wa kwanza ilikichaguliwe kuwa kikundi mama.

Mafunzo

Kama kikundi cha TIST mtapatiwa mafunzo yatakayo wawezesha kumudu nyanja mbalimbali za TIST. Ndani ya mafunzo hayo mtapata utunzaji na uendelezaji wa kitalu cha mbegu, kutayarisha udogo, mbinu za upandikizaji inavyotakiwa ndani ya kikundi, kutambua na kuchangia njia Bora, utunzaji na uhifadhi wa fedha Bank, matumizi ya skana (Kompyuta) na teknolojia nyinginezo, mbinu za hifadhi katika kilimo, na masuala mmengine mengi. Mafunzo yatatolewa na waratibu wa TIST wa eneo lako, waratibu wengine wa TIST wa kutoka eneo jingine kote duniani. Baadhi ya shughuli za mafunzo zitatolewa katika kituo na mafunzo mengine yatatolewa vijijini. Mafunzo yatatolewa kwa wanavikundi au kwa wawakilishi kutoka ndani ya kikundi kwa msingi wa kupokezana mmoja baada ya mwingine. Mtakuwa mkijulishwa juu ya mihura ya mafunzo kwa njia ya magazeti au jarida, moja kwa moja na mratibu wa TIST au ndani ya uongozi wa vijiji.

Hongera tena kwa mara nyingine na karibu TIST.

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania The International Small Group and Tree Planting Program Karatasi Zenye Kuelezea Ukweli Halisi Juu Vikundi Vya TIST

Yaliyomo:

Karatasi za ukweli halisi ni mkusanyiko wa uzoefu wa vikundi vya TIST. Yaliyomo yanaweza kubadilika kwa kadri taarifa nyingi zinavyozidi kukusanywa kutoka kwenye vikundi hapo baadaye.

Yameandikwa kwa ajili ya vikundi vidogo vidogo viweze kutumia na hata kwa wezeshaji wa maeneo husika kuweza kutumia wakati wa mafunzo yao.

Kila taarifa inajumisha kipengele cha “Uamuzi wa Kikundi” kipengele hichi kina maswali ambayo wanakikundi wanatakiwa kujadili na kufikia muafaka wao wenyewe.

Karatasi hizi zenye kuelezea ukweli halisi juu ya vikundi vya TIST zitakuwa zikitolewa moja kwa moja mkono kwa mkono kama kurasa moja yenye taarifa kwenye vikundi.

1.0 VIKAO VYA VIKUNDI VIDOGO VIDOGO

1.1 MAANA YA KIKUNDI KIDOGO

Kikundi kidogo ni muungano wa watu 6 hadi 10 na wasio zaidi ya 12 ambao watakuwa wamekubaliana kwa madhumuni ya kuwa pamoja na kusaidiana na kufanya kitu walichokubaliana. Kikundi pia kinaweza kukubaliana kukua kiroho na hata kuwafikia watu wengine nje ya kikundi.

1.2 JINSI YA KUENZISHA KIKUNDI

- Kutafuta jina la kikundi
- Kutengeneza makubaliano kwa kikundi ambayo yataonyesha matazamia, uthamani na tabia za kikundi kinataka kiweje. Andika kwenye karatasi. Kila mmoja kwenye kikundi anatakiwa kusaini makubaliano hayo.

1.3 VIKAO VYA KILA WIKI

- Kukutana kila wiki angalau kwa masaa mawili.
- Lazima kuwe na mwezeshaji na mwezeshaji mwenza kwa kila kikao. Katika kila kikao, mwezeshaji na mwezeshaji mwenza lazima wawe wanakikundi tofauti tofauti katika kikundi hicho.
 - Kila kipindi mwezeshaji ni mtendaji wa kukundi, na si “bosi” “Mwenyekiti” au “Mwalimu”. Yeye ni mtumwa na husaidia wanakikundi wanapokuwa wanajadili na kukubalina juu ya shughuli fulani. Mwezeshaji lazima awe mnyenyekevu, anayekubalika, mvumilivu, mwaminifu na muwazi. Mwezeshaji kila kipindi anapaswa kuwatia moyo wengine waongee kuliko yeye ndiye kuwa muongeeji mkuu.
 - Mwezeshaji mwenza humsaidia mwezeshaji kutunza muda wakati wa kikao na kumsaidia mwezeshaji na kikundi katika njia yoyote inahitajika.
- Uwezeshaji / Uongozi wa mzunguko katika kila kikao kwa kila wiki. Hii ni muhimu sana. Uongozi wa mzunguko humpa kila mtu nafasi ya kuwa mwezeshaji na mwezeshaji mwenza. Kila mwanakikundi atakuwa na nafasi kuonyesha kipawa chake kwenye kikundi, na atapata uzoefu wa kujiamini kama mwezeshaji mtendaji.
- Kuwa na ratiba kwa kila kikao cha kikundi.
 - Vikao ni lazima vianze na kuisha kwa wakati uliopangwa (KUMBUKA: HII HAITAKUWA KILA MAHALI)
 - Mwanzoni mwa kila kikao, kikundi ni lazima kikubaliane kwa mara nyingine juu ya shughuli za kikao hicho, na kufanya mabadiliko katika ratiba kama ikihitajika.
- Kuwa na muda wa “Kujengana” mwishoni mwa kila kikao cha kikundi.

- Hakikisha kuwa ratibu muda wa suala hili.
- Kila mtu katika kikundi lazima aseme kitu maalum, chenye manufaa juu ya mwezeshaji wa kikundi alichokifanya wakati wa kikao au ni jinsi gani mwezeshaji amejionyesha. Hii si hiari.
- Baada ya jambo hilo, akipenda, mwanakikundi yeyote anaweza kusema kipawa chochote maalum ambacho mwezeshaji anacho na amekionyesha wakati wa kikao. Hii ni hiari.
- “Kujengana” hufanya kazi bega kwa bega na uongozi wa mzunguko kwa uwezeshaji wa vikao. Pia huwafunza wanakikundi kuangalia mambo mazuri, na kuyasema. “Kujengana” pia hufundisha kikundi kufikiri ni jambo gani la muhimu katika uwezeshaji. Kila mwezeshaji mpya manufaa ya kujifunza “Kujengana” kutoka kwa mwezeshaji aliyepita.
- Mwezeshaji na mwezeshaji mwenza katika wiki wanahitajika kupanga nafasi kwa ajili ya kikao cha kikundi.
 - Kukaa katika mduara wa kubanana.
 - Kusiwe na meza mbele ya mwezeshaji au mwezeshaji mwenza na hata kwa wengine. Kwa inatakiwa kuwa hivyo lakini inaweza kuzuia mawasiliano.
 - Chagua wimbo na kuanza kuimba wakati wanakikundi wanapokusanyika pamoja.

1.4 UAMUZI WA KIKUNDI

- Ni siku zipi za kukutana?
- Wapi mahali pa kukutania?
- Ni mambo gani makuu mnataka yafanyike katika kikundi chenu, mbali na upandaji miti?

2.0 MBEGU NA AINA ZAKE

2.1 KUCHAGUA MBEGU

- Chagua mbegu na aina za miti ambazo wanakikundi wenzio wangependa kuwa nazo na ambazo zitahimili kwenye hali ya hewa ya eneo lililopo. Baadhi ya aina za miti ambazo unaweza kuzitafuta ni zile ambazo :
 - Hutoa kimvuli kwenye nyuma yako au shambani mwako
 - Huzuia upepo kwenye nyumba yako
 - Kutengeneza fensi nzuri ya kupendeza kuzunguka nyumba yakao au shamba na hata kanisa
 - Hutoa matunda, mbegu za karanga na mafuta
 - Hutupatia madawa na madwa ya kuulia wadudu
- Kuchagua aina za miti ambazo ni nzuri kwa eneo lako.
 - Pata aina ya minti ambayo wanakikundi wenzio wanafahamu kuwa inakuwa vizuri katika eneo lenu.
 - Hakikisha kuwa aina hiyo ya miti inakuwa vizuri hata bila mvua nyingi kama upo kwenye eneo kame.
 - Hakikisha kuwa miti imekuwa katika eneo lako kwa muda mrefu. Usitumie kitu ambacho ni kipya kutoka katika nchi nyingine au ardhi nyinginekwa sababu inaweza kuwa si nzuri kwa eneo lako. Unaweza kujaribu baadhi tu kwa majaribio kuona kama inawezekana. Jaribu chache kwa jaribio.
 - Chagua aina za matunda na miti yenye mbegu za karanga. Unaweza kula au ukauza matunda na mbegu za karanga.
 - Chagua miti ambayo magamba yake hutumika au matawi yake kutumika kwa mbao.
 - Chagua aina ambayo inaweza kudumu kwa muda mrefu. Watoto wako na wajukuu zako waweze kunufaika faida ya kazi yenu mnayoifanya sasa! Afisa misitu anaweza kukupa juu ya aina za miti.
- Kuna njia tatu za kupata mbegu au miche:

- Chuma mbegu zilizokomaa kwenye mti unaotaka kupanda. Hii haina gharama bali inachukua muda mrefu. Unaweza ukawatumia watoto wakakusaidia juu ya jambo hilo. Uwaonyeshe ni jambo gani walifanye.
 - Nunua mbegu kutoka kwa maafisa misitu na makampuni ya mbegu. Buy seeds from forestry officers and seed companies. Angalia tarehe ya mwisho ya kuharibika mbegu yako na hakikisha mbegu zinapandwa kabla ya tarehe hiyo.
 - Nunua miche kutoka kwenye vitalu. Nunua miche kutoka kwenye vikundi vingine. Unaweza kununua miche ikiwa kwenye viriba vyake.
- Muhimu: Fuatilia kwa maafisa misitu wa eneo lako ni aina gani ya miti husaidia mimea kukua kabla hujapanda miti karibu na shamba lako. Baadhi ya aina ya miti huzuia mimea mingine kuota karibu yao. Na mingine husaidia mimea kukua vizuri.

2.2 UAMUZI WA KIKUNDI

- Ni aina gani ya miti unatakukuza? Ni miche gani itakuwa vizuri karibu na mimea?
- Ni nani atakaye safirisha miche?
- Ni njia ipi bora ya kuiwezesha kila aina ya mbegu kuota?
- Ni kwa jinsi gani mtahakikisha mnapata miche au mbegu nzuri yenye afya.

3.0 KUENDELEZA NA KUTUNZA VITALU.

3.1 CHAGUA ENEO.

- Chagua eneo la kitalu ambalo lipo mahali ambapo pa uwazi ambapo kuna mwanga wa jua lakini penye kivuli na mahali ambapo ni tulivu. Hii inaiepusha mimea kupata joto la kutosha na hata mvukisho wa maji.
- Eneo ni lazima iliwe mahali pazuri kwa kujali na kuitunza miche mingi kwa pamoja.
 - Chagua eneo lenye mtelemko kiasi, ambapo itakuwa ni njia ya kutoka kwenye maeneo yenye matatizo ya mafuriko.
 - Chagua eneo ambalo lipo karibu na maji kama vile mto, ziwa, maji ya kupampu, kisima au chemichemi.
 - Chagua eneo ambalo linafikika kiurahisi.
 - Chagua eneo / Mahali ambapo ni karibu na pia mahali ambapo miche itapandikizwa.
 - Chagua eneo ambalo lipo mbali na mahali pa mifugo na kuchezea watoto.

3.2 MAANDALIZI YA ENEO NA UPANDIKIZAJI WA MBEGU

- Chambua ni mbegu zipi za kupandikiza kwenye viriba na ni zipi za kupandikiza kwenye majaruba. Pata msaada kutoka kwa afisa misitu wa eneo lako.
- Chambua kama kuna mbegu zinazohitaji kufanyiwa marekebisho kabla ya kupanda. Pata msaada kutoka kwa afisa misitu wa eneo lako.
 - Mbegu za kundekunde zina magamba ya nje magumu ambayo hufanya hewa na maji kushindwa kupenya kwenye sehemu ya ndani ya mbegu. Mbegu hizi zinahitaji kurekebishwa, kama vile kwa kuzichemsha kwa maji ya moto, kuondoa gamba la juu kwa kutumia kifaa maalum n.k.
- Andaa udongo kwa kuchanganya sehemu 3 za udongo wa tabaka la juu kutoka msituni, sehemu 2 za udongo wa kichanga na sehemu 1 ya mbolea. Hakikisha unatengeneza wa kutosha.
- Andaa chombo cha kupandikizia mbegu.
 - Kusanya viriba vyote vya zamani na vikombe viliharibika vilivyozagaa kuzunguka nyumba yako na kijiji ambavyo vitatumika kama vyombo vyombo vya kupandikizia mbegu. Hii pia itasaidia kuondoa uchafu, kuweka kijiji chenu katika hali ya usafi.
 - Kama una viriba vikubwa au makaratasi, vikate kate katika vipande vidogo vidogo vyenye urefu wa sm 24 na kikunje nusu. Kishoneleze hadi kupata urefu wa sm 13. Hii itafanya kupata uwazi wa mduara wenye ukubwa wa sm 24.
- Kwa mbegu zinazohitajika kupandikizwa kwenye viriba:

- Jaza kiriba kwa udongo ulio andaliwa ..
- Weka mbegu ambazo zinatakiwa kupandwa kwenye kiriba katika udongo.
- Weka udongo zaidi juu ya mbegu mpaka angalua mara mbili ya unene wa mbegu.
- Acha angalau sm 5 za kiriba wazi kwa juu kuruhusu maji kutwaama wakati wa umwagilaji.
- Kwa mbegu zinazohitaji kupandikizwa kwenye kitaru:
 - Andaa jaruba kwa kutumi matofali au mawe lenye upana wa mita 1 na urefu kutegemeana na kiasi cha mbegu amazo zitapandikizwa.
 - Jaza jaruba kwa chini na tabaka la mawe yenye upana wa sm 5 (au weka tabaka la nailoni kwa chini) kabla ya kuweka udongo ili kuzuia mizizi kupenya na kujikita ardhini kama aina ya miche ina mizizi mirefu.
 - Halafu lifuatie tabaka la udongo ulio andaliwa kwa upana wa sm 10.
 - Kwa tabaka la juu, tumia mchanga lainiambao vumbu na matope yameondolewa, fanya tabaka hili liwe na upana wa sm 5.
 - Mbegu ni lazima zipandwe kwenye jaruba na machanga kwa juu hadi kufikia angalau mara mbili ya unene wa mbegu. Usijaze jaruba pembezoni kwa kuwa itasababisha mchanga na mbegu kusambaa wakati wa kumwagila.
- Rekodi aina za miti ulizopanda kwenye viriba na kwenye jaruba.
- Hesabu zilikwisha pandikizwa hata kama hazijaota na andika tarehe ya kusiha mbegu.
- Panga viriba katika mistari na katika makundi ya 100, 200, au 500, utakavyopendekeza. Pangilia kutokana na aina za miti ili iwe rahisi kwa Kwantifaya (Mhesabuji) kurekodi taarifa yake kwa aina.
- Baadhi ya mbegu zinaweza kushindwa kuota na baadhi ya miche inaweza kufa. Kwa hiyo, pangilia mahesabu ya juu na kupanda miche zaidi kuliko ile idadi unayotarajia kupanda katika eneo lako.

3.3 MATENGENEZO YA VITALU

- Mwangilia miche mara kwa mara. Uwe mwangalifu usimwagie maji mengi kupita kiasi..
- Wakati wa msimu wa mvua, funika miche kwa kutumia majani makavu. Miche ni lazima iondolewe kutoka chini ili kwamba maji yasichuruzikie kwenye miche.
- Kumbuka kwamba wakati wa kuotesha anatoftiana kutoka aina moja ya mti na nyingine. Baadhi huota kwa muda mfupi na nyingine huchukua wiki kadhaa.
- Kama aina fulani haioti ndani ya kipindi cha kawaida basi pandikiza tena viriba hivyo na maeneo ya majaruba.
- Angalia uwepo wa wadudu na magonjwa.
 - Nyunyizia dawa za asili na za kisasa pale inahitajika.
 - Mfano mzuri ni kutumia maji machungu yatokanayo na kuchemsha majani ya muarobaini kama dawa ya kuangamiza wadudu.
- Hamisha hamisha viriba mara kwa mara.
- Kata mzizi wowote unaojikita ardhini.
- Zungushia wigo kitalu chako ili kukilinda na mifugo na watoto kuchezea.
- Acha miche ikue hadi kufikia sm 30 kabla ya kupandikizwa. Hii inaweza kuchukua kuanzia mwezi 1 hadi miezi 6.

3.4 UAMUZI WA KIKUNDI

- Kikundi kitakuwa na vitalu vingapi? Kila mwana kikundi atakuwa na cha kwake, au wanakikundi wote wana kitalu kimoja au njia zote mbili zimetumika?
- Je vitalu vitakuwa wapi?
- Ni jinsi gani kikundi kitashughulikia umwagilaji na kuitunza miche?

4.0 KUANDAA ENEO LA KUPANDA MITI

4.1 MAHALI PA KUPANDA MITI

- Chugua eneo la kupanda miti mahali ambapo watu watanufaika kwa muda mrefu:
 - Mipaka ya shamba: Tumia miti kama alama za mipaka ya shamba lako na kuinga mimea kutokana na upepo.
 - Njia: Miti inaweza kuweka njia na kuweka kimvuli.
 - Kuzunguka nyumba: Unaweza kupanda miti kufuta njia na pia kuweka kimvuli.
 - Kuzunguka mimea: Baadhi ya aina za miti inaweza kuzuia mmomonyoko wa udongo katika tabaka la juu la ardhi. Baadhi ya aina ya miti inaweza kuleta virutubisho kwenye udongo ili kusaidia ukuaji wa mimea.
 - Kwenye mashule, makanisa na hata kwenye majengo mengine ya umma miti inaweza kupandwa na kuleta kimvuli na kuupendezesha ardhi.
- Chagua eneo ambalo lipo wazi.
- Epuka kutumia mashamba makubwa.
 - Mashamba mengi makubwa kuwa na aina za moja au mbili tu za miti: Hii inaweza kuungua na moto na kuharibiwa na wadudu.
 - Ardhi inaweza kuwa na matumizi mengi, si kwa ajili ya kupanda miti tu.
 - Aina nyingi za miti zinatakiwa kupandwa ili kuboresha ardhi.
 - Mashamba mara nyingi huwa hayapaswi kuwa karibu karibu sana makazi ya watu ili kuwa na ugumu wa watu kwenda kukusanya kuni, matunda na mbegu za karanga na hata ma maganda.
 - Kupanda miti mingi sana ya aina moja inaweza kuunguzwa na moto au hata kuliwa na wadudu.
 - Baadhi ya wanyama wanaweza kuishi kwenye eneo hilo ulilopanda miti na hivyo kuwa tatizo.
 - Serikali ya kijiji inaweza kuamua kutumia aneo mlilokwisha kupanda miti kwa shughuli nyingine, kama vile kujenga shule au Zahati.
 - Watu wasiowanakikundi wanaweza kukata miti au kusanya kuni.
- Baadhi ya vikundi vinapanda miti yao kwenye groves (bustani ya miti) kwa sababu:
 - Wanaishi mjini na kwenye nyumbani za kupanga na hawana mashamba yao wenyewe.
 - Wanataka kupata miti mingi katika eneo moja na kufikiria kuwa itakuwa ni rahisi kuitunza.
- Kama ukipanda katika shamba kubwa:
 - Panda aina za miti 10 au zaidi katika eneo lililo kubwa.
 - Tengeneza makinga moto kuzunguka shamba lako kwa kuchimba na kuondoa majani pembezoni mwa shamba lako.
 - Kufikiria kupanda miti kwa umbali wa futi 8 kutoka mti mmoja hadi mwingine. Kama mkipanda karibu zaidi ya hapo, hii inaweza kusababisha baadhi ya miti kufa na mingine kudhoofika.
 - Kuwa na shamba la miti karibu na kijiji, kutawezesha wanakikundi kwenda na kupata mahitaji yao ya kuni, matunda, mbegu za karanga na magamba ya miti.
 - Wood lots can be used to raise trees for sale. Make sure the wood lots are close to where the people can come and buy wood.
- Kama wanakikundi hawamiliki ardhi, basi hakikisheni kuwa mnapata ruksa kabla ya kupanda miti.

4.2 KUANDAA ENEO

- Ondoa vichaka na magugu.
- Acha mti wowote ambao una nguvu na afya njema.
- Ondoa miamba pale ambapo utapanda miti.
- Mwishoni mwa msimu wa mvua, andaa mashimo kwa ajili ya kupanda miti msimu ujao. Kuchimba mashimo katika ardhi iliyonyeshewa ni laini kuliko ile ardhi iliyo kame. Mashimo

yanaweza kufukiwa udongo kabla msimu wa mvua kunyesha lakini itakuwa rahisi kulichimba tena.

- Kuchimba mashimo marefu, na ya mraba.
 - Uliza maafisa misitu na wanakikundi wengine ni ukubwa gani wa mashimo ni mzuri na umbali kiasi gani kutoka mti mmoja hadi mwingine. Mpwapwa, mashimo yanapaswa na ukubwa wa futi 2 upana na 1 1/2 urefu kwenda chini.
 - Weka mashimo umbali wa shimo hadi shimo futi 12. Kama miti itatumika kwa mbao, mashimo yanapaswa kuwa karibu karibu (Kama futi 8 hadi 10).
 - Usiyapange mashimo katika mstari mnyoofu. Hii inaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo.
 - Jaribu kuwa na idadi sawa ya mashimo kwa kila mstari, ni rahisi kuhesabu miti iliyopandwa.
 - Tenganisha udongo wa tabaka la ardhi la juu na ule wa chini, udongo wa kichanga na tifutifu. Weka udongo wa juu.
 - Uwe mwangalifu kwamba mashimo yanachimbwa kiasi kwamba maji ya mvua yanaweza kuingia kwenye shimo. Kwa mfano, kingo kubwa iliyoinuka kwa juu kutoka kwenye mti inaweza kuzuia maji ya mvua yasiingia kwenye shimo.
- Kiasi cha wiki 4 hadi 6 kabla ya kupanda miti, andaa udongo kwa ajili ya kupandia.
 - Changanya udongo wa tabaka la juu na mbolea za samadi, au mboji (kata na kusanya mbegu za magugu halafu yafukie chini.)
 - Changanya udongo wa tifutifu na ule udongo wa chini na mbolea ya mboji na halafu lijaze tena shimo, weka udongo wa juu /mbolea katika tabaka la juu la ardhi (sehemu ambapo miche itapandikizwa.)
 - Acha sm chache katika shimo bila kufukia kwa juu ya shimo ili kukusanya na kuvuna maji.
 - Weka mti katika ya shimo ili kuweka alama katika ile sehemu ya kupanda mti.
 - Ondoa takataka zote katika eneo la mtelemko la shimo ili kwamba maji ya mvua yaweze kwenda kwenye shimo.
 - Panga na wanakikundi wenzio kufanya shughuli hii kabla ya muda wa kupandikiza miti! Kwa njia hii kazi yoyote ile iliyo ngumu inafanywa kuwa rahisi.

4.3 UAMUZI WA KIKUNDI

- Ni nani atakaye ondoa vichaka na miamba na magugu? Na ni lini itakapofanyika?
- Ni nani atakaye chimba mashimo wakati ardhi ikiwa bado mbichi/ imelowana kutokana na mvua.
- Kama hakuna mboji au mbolea ya samadi karibu, na ni nani atakayesambaza?

5.0 KUPANDIKIZA MICHE

5.1 KABLA YA UPANDIKIZAJI

- Miche yenye afya na yenye urefu wa sm 30 au zaidi ya hapo ni mizuri kwa kupandikizwa na inatakiwa iondolewe ipelekwe kwenye eneo la kupanda miti.
- Sogeza miche karibu na eneo lako la kupanda miti wiki 1 au 2 kabla mvua hazijaanza kunyesha, kama kuna uwezekano basi mwagilia miche wakati ukiwa unasubiri mvua. Hii ina rahisisha usafirishaji.
- Pandikiza miche katika mashimo kabla ya wiki 2 na si zaidi ya hapo au wiki mbili baada ya mvua kuanza kunyesha ili kuhakikisha kuwa miche yako inafaidika kadri mvua inavyonyesha.

5.2 UPANDIKIZAJI

- Maandalizi ya udongo: hakikisha kuwa udongo wa juu na ule wa chini unatenganishwa, changanya na mbolea, na kuurudishia kwenye shimo. Ondoa udongo uliolundikwa ili kuruhusu maji ya mvua kuweza kuingia kwenye shimo.
- Ondoa viraba kutoka kwenye mche.
 - Uwe mwangalifu usipoteze kiriba ili uweze kukitumia kwa mara nyingine.
 - Na kama ni lazima kukatwa, basi kata kamstari kadogo tu ili uweze kuparudishia baadaye.
- Vuta udongo pembeni, weka mche kwenye shimo.
- Weka takataka kuzunguka mche.
 - Kama kuna chupa tupu ya lita , kata kitako chake, ondoa kifuniko, na uiweka huku ikiwa upande wake wa ugeuziwe chini, kuelekea kwenye mizizi.
 - Weka takataka kuzunguka mche na chupa ya maji.
- Shindilia kuzunguka mche kikamilifu mara 8 au hata mara 10.
- Mwagilia mche.

5.3 BAADA YA KUPANDIKIZA

- Weka vijiti kuzunguka mche ili watu waweze kuona ili wasije kupita juu yake.
- Weka miti ya vichaka na matawi ya miba kuzunguka eneo liliopandwa ili wanyama wasilivamie.
- Ondoa magugu yote kuzunguka mche kila baada ya wiki 2 hadi 3.
- Mwagilia miche mara moja kwa wiki kama hakuna mvua za uhakika.

5.4 UAMUZI WA KIKUNDI

- Ni njia zipi bora za kuwa unganisha wanakikundi ili kupata muda wa kumwagilia na kupalilia miti?
- Ni jinsi gani kikundi kinaweza kuitambua miti yake na kuitunza isiharibiwe na wanyama na watu?

**Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania Ltd.
The International Small Group And Tree Planting Program
FOMU YA KUANDIKA SHUGHULI ZA KIKUNDI**

Vikundi vinapaswa kuweka kumbukumbu vizuri. Kikundi kinapaswa kuweka kumbukumbu katika kitabu maalum. Rekodi habari zifuatazo katika kitabu cha kumbukumbu. Kama hakuna shughuli au taarifa, basi kikundi kinatakiwa kuandika kwenye kitabu cha kumbukumbu kwamba hakuna "shughuli au taarifa zilizofanyika.

1. Tarehe ya kukutana
2. Idadi ya wanakikundi waliohudhuria
3. Jina la mwezesaji
4. Jina la mwezesaji mwenza
5. Muda wa kikao
6. Hatua zilizochukuliwa
 - a. Juu ya kitalu au upandaji miti
 - b. Katika shughuli nyingine
 - c. Juu ya kitalu au upandaji miti
 - d. Katika shughuli nyingine
7. Ni miche mingapi iliyoongezeka wiki hii
8. Ni miti mingapi iliyopandwa wiki hii
9. Miti mingapi iliyokutwa imekufa wiki hii
 - a. Ukuzaji na Upandaji wa miti
 - b. Maendeleo ya vikundi
10. Ni kiasi gani cha ardhi kimepatikana au kuandaliwa wiki hii kwa ajili ya kupanda miti
11. Shughuli za kuandaa kilimo Hai Wiki hii
12. Idadi ya Ekari zilizotayarishwa kwa ajili ya Kilimo Hai
13. Njia Bora Mpya zilizopatikana katika:
 - a. Upandaji miti na ukuzaji wa miti
 - b. Uendeshaji wa vikundi
 - c. Kilimo Hai

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd.
The International Small Group and Tree Planting Program
TAARIFA YA MWEZI YA KIKUNDI.

Maelekezo: 1.) Jaza fomu hii kila mwisho wa mwezi. 2.) Jibu maswali ya mwezi yale yanayomalizikia 3.) Rudisha kwa Mratibu wako wa TIST. Asanteni sana.

Namba ya TIST	Mwezi: _____ Mwaka: _____
Jina la Kikundi	
Kijiji	
1. Tarehe ya kukabidhi fomu hii	
2. Mwezi na Mwaka wa Taarifa hii	Mwezi: _____ Mwaka: _____
3. Jumla ya vikao vinavyofanyika	Zungushia idadi ya vikao 0/ 1/ 2/ 3/ 4/ 5
4. Idadi ya wanakikundi katika kikao cha mwisho	Wanakikundi _____
5. Idadi ya wanachama wa kikundi mwishoni mwa mwezi huu	Wanakikundi _____
6. Mlitumia muda gani katika kikao cha mwisho?	Dakika _____
7. Mara ya mwisho kikundi kukutana ni tarehe ngapi.	
8. Ni wawezeshaji mbalimbali wangapi walioweza mwezi huu?	Zungushia au: 0/1/2/3/4/5
9. Ni miti mingapi iliyokufa mwezi huu?	Miti iliyokufa _____
10. Idadi ya miche iliyo hai mwishoni mwa mwezi huu.	Jumla ya Miche kwenye vitalu _____
11. Ni miti mingapi iliyokuwa hai hadi mwisho mwa mwezi huu?	Jumla ya Miti iliyopandwa iliyo hai _____
12. Ni ekari ngapi zilizotayarishwa na Wanakikundi kwa ajili ya Kilimo Hai	Idadi ya Ekari _____
13. Je Kikundi chenu kimepata Jarida la HMM mwezi huu?	Zungushia au: Ndiyo/Hapana
14. Kikundi chenu kimepokea hati ya malipo mwezi huu?	Zungushia au: Ndiyo Hapana
15. Kuna mfanyakazi wa TIST aliyekuja kuhesabu miti yenu mwezi huu?	Zungushia: Ndiyo/Hapana TAREHE
16. Kuna Akaunti iliyofunguliwa au kubadilishwa mwezi huu	Zungushia au: Ndiyo/Hapana
17. Kama kuna namba mpya ya akaunti, ni ipi hiyo?	Namba ya Akaunti: Tawi la Bank: _____
18. Je mna Njia Bora yeyote ambayo mngpenda watu wengine wajaribu? Tafadhali andika nyuma ya fomu hii.	
19. Je mna mawazo yeyote mapya kwa ajili ya kuboresha mradi? Andikeni mawazo hayo nyuma ya fomu hii.	
Sahihi za wanakikundi 4 kudhihirisha kuwa Taarifa ya kikundi ni sahihi kabisa	1. _____ 2. _____ 3. _____ 4. _____

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd.
The International Small Group and Tree Planting Program
Small Group Account Statement and Payment Voucher

Taarifa ya Fedha ya Kikundi Kidogo cha TIST

TIST Small Group Financial Statement

Kutoka Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania Ltd. (UMET)/CAAC

From UMET/CAAC

Jina la Eneo la Kikundi: GCName <i>Group Center Name:</i> Kijiji: _____ <i>Village:</i> Jina la Kikundi: Jerusalem <i>Group Name:</i>	Eneo la Kikundi: GCCode <i>Group Center Code:</i> Namba ya Kikundi: 123 <i>Group Number:</i> Tarehe ya Tarifa: 1 Jan 2003 <i>Statement Date:</i> Kwa: Oct – Dec 2002 <i>For:</i>
--	---

Malipo ya miti ambayo bado hayajalipwa:

Tree Payments Outstanding:

Tarehe Date	Miche Seedlings	Miti Trees	Jumla Total		Malipo Payment	Taarifa Iliyotumwa Reports Submitted
Oct-Dec 2002	1250	2000	3250	X 4/=	13,000/=	

Jumla: 13,000/=

Total:

UMET italipa malipo ya miti mara tu fomu 3 za ripoti ya mwezi zitakaporudishwa katika kipindi cha miezi 3 kwa mtiririko na Kutoa taarifa kuwa kikundi kimefungua Akaunti katika Tawi gani na jina la Benk. Benk mpya na badiliko lolote la Benk inaweza kutolewa kupitia fomu za ripoti ya mwezi.

UMET pays the above amount once 3 monthly reports in a given 3 month period have been submitted and a bank branch has been chosen. New and changed bank details can be submitted on your next monthly report form.

Jumla ya Fedha Iliyupo kwa Ajili 13,000/=

ya Kuwekwa Benk Sasa:

Total Payment Now Available for Bank Deposit:

Vocha

Namba ya Vocha: GCCode-123-01-01-2003

Voucher Voucher Number:

Kiasi Kilichowekwa Benki: 13,000/=

Amount Payable for Deposit at Bank

Jina la Akaunti: _____ Namba: _____ Tawi: _____
Account name: Number: Branch:

Walipwaji fedha taslim: 1. _____, 2. _____, 3. _____
Group Names to receive cash:

Sahihi: 1. _____, 2. _____, 3. _____
Signatures:

Benki imeidhinishwa kutoa fedha toka kwenye Akaunti ya UMET Ltd, na kuweka au kugawa kufuatana na maelekezo ya hapo juu.

The Bank is authorized to withdraw funds from the UMET Ltd. Account and deposit or distribute according to the requirements above.

Jina la Akaunti: UMET Ltd. Namba: _____ Tawi: _____
Account name: Number: Branch:

Sahihi ya Mwakilishi wa Benki Tarehe

Bank Representative Signature Date

UMET Ltd. (CAAC), c/o Nasser and Co., Box 22731, Dar Es Salaam, Tanzania

Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania Ltd. The International Small Group and Tree Planting Program (TIST) Greenhouse Gas Sale Agreement

Kikundi: _____ Kijiji: _____
Namba ya Kikundi cha TIST: _____ Wilaya: _____
Namba ya kituo Cha Kikundi cha TIST: _____ Mkoa: _____

Kikundi hiki kidogo kitatoa hati hewa chafu iliyokusanywa (ERCsw) kwa UMET kila mwaka wakati mkataba huu unafanya kazi. UMET italipa vikundi shilingi 4 kwa mti kila robo mwaka wakati mkataba huu unafanya kazi.

MISAMIATI NA MAAIMISHO KATIKA MKATABA HUU

1. CO2 ni hewa chafu (GhG) ambayo inatakiwa iondolewe angani/hewani.
2. Kupanda miti kunaondoa hewa chafu (CO2) angani na kuihifadhi kama Carbon kwenye mizizi, mashina na matawi yake.
3. Kilimo endelevu (njia bora za kilimo) pia zinaondoa hewa chafu angani na kuihifadhi ardhini kama Carbon.
4. Hewa chafu iliyoondolewea hewani yawezwa kupimwa na kugeuzewa hati ya dhamana (ERCs), ambayo inawezwa kuuzwa.
5. UMET italipa vikundi vidogo ili kuondoa hewa chafu (CO2) hewani na kuihifadhi kama Carbon kwenye miti na nardhini.
6. Kwa miaka 20 ya kwanza ya mkataba huu, UMET italipa vikundi vidogo kutokana na idadi ya miti iliyo hai ambayo kikundi kidogo kitakuwa nayo mwisho war obo mwaka. Mwishoniwa robo mwaka, vikundi vitahesabu miti iliyo hai waluyanayo na kujaza kwenye fomu na kuipeleka UMET iliwa imekamilika na kutiwa saini/sahini. UMET italipa vikundi shilingi 4 kwa mti, kulingana na fomu ya ERC na marekebisho yoyote muhimu yatakayofanywa na UMET au wakaguzi.
7. Baada ya miaka 20, UMET itaendelea kulipa nusu ya miti katika kiwango cha shilingi 4 kwa mti ulio hai kwa robo mwaka, na kulipa nusu ya ERCs zilizokusanywa kwa mwaka. Katika kiwango cha bei ya soko la dunia itakayowekwa makati wa maadhimisho ya miaka zo ya mkataba huu, na kila maadhimisho ya miaka 10 baada ya hapo, kulipa gharama ndogoxz zitakazotokana na uthaminishaji, uthibitishaji na uuzaji wa ERCs.
8. Vikundi vinamiliki miti, matunda, madawa na mazao yote yanayotokana na miti. UMET na wauziwaji, wao watamiliki haki ya kuhufadhi Carbon, yaani CO2 ERCs. Kama kikuni kinakata miti, hewa ya Carbon inapotea na kwa sababu hiyo CO2 ERCs zilizokusanywa kutokana na miti iliyokatwa zitapotea/zitafutwa. Vikundi havipaswi kukata miti, wala kutumia miti kwa ajili ya kuni au mbao, isipokuwa tu kama vinaendeleza njia bora za kilimo cha misitu kama vile upogaoaji wa miti/kukatia matawi yasiyohitajika.
9. Ili CO2 ERCs ziwe na thamani, ni lazima zithibitishwe na kikundi kidogo, UMET, na iliwezekana na mkaguzi mwingine. ERC yawea kuthibitishwa kama:
 - a. Taarifa zinaonyesha kwamba upandaji miti na kilimo bora ulianza baada ya tarehe 1 Januari, 2000.
 - b. Wachukua takwimu za miti (quantifiers) wa UMET na wathibitishaji wa nje wataweza kuhesabu miti katika maeneo yaliyotajwa na vikundi vidogo, na kama watathibitisha vikundi vimekuwa vikitumia njia bora za kilimo.
 - c. Vikundi vitasaini fomu kuthibitisha nimiti mingapi iliyo hai, na hekta ngapi kikundi kilitumia kwa ajili ya njia bora za kilimo endelevu.
 - d. Taarifa za vikundi zinathibitisha kuwa kikundi kilipanda miti, na kuitunza isiharibiwe.
10. UMET itahesabu ni kiasi gani cha Charbon kilichohi- fadhiwa ili kithibitishwe, na ili ERC ziuzwe.

MAMBO YA KUFANYWA

A. Kikundi Kidogo

1. Kitapanda miti na kuitunza hadi itakapokomaa. Miti mingine itaishi zaidi ya miaka 100!
2. Wanakikundi watatekeleza kilimo endelevu walau kwa kila mwanakikiu-ndi kuwa na ekari moja.
3. Kupandikiza miti migine kama ile iliyopandwa itakufa, itachomwa moto, au kuharibuiwa na wanyama au watu kila mwaka kwa miaka 20.
4. Kitatoa hati za hewa chafu iliyo kusanywa na UMET kwa UMET tu na wala si kwa mnumuzi mwingine.
5. Kitashiriki kwenye mafurizo na programu nyingine za TIST kusaidia kubuni na kutumia njia bora (za kilimo na upandaji miti).

6. Kutoa HATI nii ya mkataba, na ERCs za baadaye zitakazotokana na shughuli za kikundi, na kuzihamishia kwa UMET kama kikundi kitaacha kufanya kazi na UMET.
7. Kutunza taarifa za idadi ya ekari ambazo zimetunzwa kwa kutumia njia bora za kilimo endelevu, idadi ya miti iliyopandwa, lini ilipandwa, na miti iliyo hai hadi wakati huo.
8. Kuchukua wakaguzi na wadhibiti kutembelea maeneo yote ambayo miti ya TIST imepandwa (kama wataombwa kufanya hivyo).
9. Kujulisha UMET kama wanakikundi wanaondoka au wanaacha eneo ambalo limepandwa miti ya TIST.
10. Kuendelea kuwa na Akaunti ya Benki kwenye benki zilizoamriwa na UMET ili kupata malipo yao.
11. Kusaidia UMET kueleza kwa vikundi vingine namna ya kutumia kilimo endelevu, namna ya kupanda miti mingi na kuitunza ikaishi.

B. UMET

1. Italipa wakaguzi ili kuhesabu miti kwa vipindi kadha (mara kwa mara), itatunza taarifa za GhG.
2. Itatunza taarifa za usajiri wa kikundi.
3. Kuandika taarifa ya namna kikundi kinavyoshiriki katika ufundishaji, upandaji miti, na katika kilimo endelevu.
4. Kuwezesha ERCs kua kitu cha thamani ili kuuzwa kwa wanunuzi.
5. Kupata kibali cha serikali cha kuza ERCs.

KUVUNJA MKATABA

UMET yawez kuvunja mkataba huu wakati wowote na kusimamisha malipo yoyote kwa kikundi. Kama hili likitokea, vikundi vitamiliki haki ya ERCs zote ambazo hazikulipiwa na UMET.

UMET itavunja mkataba huu lakini itabakia na haki ya ERCs zote za baadae endapo kama:

1. Vikundi vinashindwa kujulisha UMET ambapo idadi ya wanachama inapungua chini ya wanachama wane (4).
2. Wamiliki ardhi wapya hawaruhusu vikundi kutunza miti na kuhamishia ERCs kwa UMET.
3. Vikundi vinakataa kutoa taarifa zinazotakiwa juu ya njia bora na kutokubaliana na programu.
4. Vikundi vimeuza ERCs zilizotokana na miti ya TIST kwa mnunuzi mwingine.

Vikundi vinaweza kuvunja mkataba huu kwa:

1. Kuhamishia mkataba huu kwa kikundi kingine.
2. Kuiandikia UMET kwamba hawajalipwa malipo yao ndani ya siku 90 tangu walipopeleka fomu ya ERC, na UMET hairekebishi malipo ndani ya siku 90 tangu ilipopekea barua kutoka kwenye kikundi kidogo ikieleza kwamba hawajapokea malipo yao.

UMET inaweza kuhamishia haki katika mkataba huu na ERCs zitakazotokea kwenye ma shirika mengine bila kushauriana na vikundi vidogo. Imesainiwa

Mwakilishi wa UMET Aliyeidhinishwa

Sahihi

Jina

Tarehe

Mwakilishi wa kikundi kidogo aliyeidhinishwa

Sahihi

Sahihi

Sahihi

Tarehe

**Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania, Ltd.
The International Small Group and Tree Planting Program (TIST)
Emission Reduction Credit Notice**

**TAARIFA YA UTENGENEZAJI WA ERC WA HEWA CHAFU CO2 UNAOFANYWA NA
VIKUNDI VIDOGO VYA TIST
KWA UBORESHAJI MAZINGIRA (I4EI) KWA MIRADI YA TANZANIA**

**Information on ERC Recipient/
Taarifa ya Mpokeaji ERC**

1. Business Name/
Jina la Kibiashera: _____

2. Company Contact/
Kampuni Mawasiliano: _____

Name/Jina	Title/Cheo	Telephone No./Namba ya Simu
-----------	------------	-----------------------------

3. Mailing Address/
Anuani: _____

Street/Mtaa

City/ Mji	Region or State/ Mkoa au Jimbo	Postal Code/ Namba ya Posta	Country/ Nchi
--------------	-----------------------------------	--------------------------------	------------------

**Information on Creation and Transfer of ERC by Small Group/
Taarifa juu ya uzalishaji na uuzaji wa ERC wa Kikundi Kidogo**

4. Group/ Kikundi: _____	5. Village/ Kijiji: _____
6. TIST Group Number/ # ya Kikundi cha TIST: _____	7. District/ Wilaya: _____
8. TIST Group Center Code/ # ya Kituo cha Kikundi cha TIST: _____	9. Region/ Mkoa: _____
11. Source Description/ Small group tree planting/ Chanzo cha Maelezo: <u>Upandaji miti wa kikundi</u>	

12. Date of Last Audit/ Tarehe ya mwisho ya ukaguzi	13. Trees Present (Last Audit)/ Miti iliyopo (Ukaguzi wa mwisho):
14. Acres of improved soil Eneolililorutubishwa (ekari)	15. Average Age of Trees/ Wastani wa Umri wa miti
16. Current Period (Year) of Sequestration/ Kipindi cha sasa (mwaka) cha uhufadhi wa CO2 ardhini na mitini	17. Metric Tons CO2 Sequestered and Transferred Tani za hewa chafu CO2 zilizohifadhiwa na kuhamishwa

**Authorized I4EI Representative/
Mwakilishi wa I4EI aliyeidhinishwa**

I am authorized by the Recipient to Receive this transfer of ERC.

Nimeidhinishwa na Mnufaika nipokee hati hii ya ERC.

**Authorized Small Group Representatives/
Wawakilishi wa kikundi walioidhinishwa**

The Small Group authorized me to sign this agreement for the Small Group to transfer ERCs to the Recipient. I reviewed the information on this form and know how it was collected. I believe it is true, accurate, and complete. I certify that the ERC come from trees owned by the Small Group. I certify that the ERCs have not and will not be transferred to anyone else except the recipient stated above. The Small Group now gives up rights to the ERCs though the Small Group still owns the trees and their ongoing sequestration.

Kikundi kidogo kimeniidhinisha nitie sahihi makubaliano/mkataba huu wa kikundi kidogo kuhamisha na kuuza ERCs kwa mpokeaji. Nimezisoma taarifa katika fomu hii na najua zilivyokusanywa. Naamini kuwa ni kweli, sahihi, na kwamba zimekamilika. Nathibitisha kwamba ERCs zimetokana na miti inayomiliki wan a kikundi kidogo. Nathibitisha kwamba ERCs hazjta hamishiwa kwa mtu yeyote isipokuwa mtajwa hapo juu. Hivyo kikundi kinaondoa haki zake kwenye ERCs ingawa bado kitaendelea kumiliki miti na kazi ya uhifadhi wa hewa chafu kwenye miti na ardhi.

Signature/Sahihi

Signature/Sahihi

Print Name/Jina (chapa)

Signature/Sahihi

Signature/Sahihi

Date/Tarehe

Date/Tarehe

FOR REGISTRY USE ONLY/ KWA MATUMIZI YA OFISI TU Reference Number Assigned by Registry/ Namba ya Rejea iliyowekwa na Msajili	
--	--